



# UZUSHI NA UKWELI

kuhusu utafiti wa tiba na kipimo cha kuchunguza kifua kikuu

UZUSHI

Watu katika nchi zinazoendelea hutumika kama “simbilisi” katika majaribio ya vipimo na tiba.

UKWELI

Utafiti wa kwanza wa kitabibu hufanyika katika nchi ambako kipimo hicho cha uchunguzi kimegunduliwa.

Baada ya usahihi wa kipimo husika kuchunguzwa katika maabara kwa kutumia sampuli, inatakiwa kipimo hicho kifanyiwe majaribio katika nchi ambako ugonjwa umeenea ili kuona kama kinaweza kubaini ugonjwa kwa watu wenye dalili za ugonjwa huo. **Kwa upande wa utafiti wa kifua kikuu, kipimo hiki kinapaswa kijaribiwe katika jamii yenye kiwango cha juu cha maambukizi ya kifua kikuu.**

UZUSHI

Damu inayochukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu baadaye huuzwa ili kupata faida.

UKWELI

Kamwe damu haiuzwi na haitumiki kwa njia zozote zisizo halali!

Damu inahitajika katika utafiti huu ili kufanya majaribio ya kipimo cha kufanyia uchunguzi. Hiki ni kipimo kipya ambacho kinabaini kingamwili kwenye damu badala ya bakteria wa kifua kikuu kwenye makohozi. Kipimo hiki ni cha haraka, na kinaweza kutumiwa katika kituo cha afya kama hiki bila kuhitaji vifaa vingine vya maabara.

**Kipimo hiki kinatumia kiwango kidogo sana cha damu. Damu nyingine itahifadhiwa kwa ajili ya kutumika baadaye kwa ajili ya kuandaa na/au kuboresha kipimo hiki, lakini hili litaweza kufanyika baada ya kupewa idhini na mshiriki.**

UZUSHI

Vipimo vinavyotumika kupima kifua kikuu huwaambukiza watu maradhi hayo ya kifua kikuu.

UKWELI

Kipimo cha kifua kikuu hakiwezi kukuambukiza ugonjwa wa kifua kikuu!

Wakati wa uchunguzi wa majaribio ya kitabibu, kiwango kidogo tu cha damu kitachukuliwa kutoka kwa mshiriki. Damu itachukuliwa kutoka katika mshipa wa damu kwenye mkono wa mshiriki kwa kutumia sindano safi na salama itumikayo mara moja na sirinji maalumu. Mshiriki atahisi “maumivu” kidogo kutokana na mchomo wa sindano, **lakini hawezi kupata kifua kikuu wala maambukizi mengine.**

UZUSHI

Ikithibitika kuwa kipimo kinafaa, hakitainufaisha jamii na wale walioshiriki katika utafiti.

UKWELI

Mara baada ya kuthibitisha kwamba kipimo kipya ni sahihi na kinafaa kutumika katika kituo cha afya kama hiki, kipimo hiki kitatolewa kwa jamii yoyote ambayo serikali yake itaridhia na kuidhinisha matumizi yake. **Dhamira yetu ni kuandaa kipimo kipya cha kifua kikuu kitakachopatikana na kutumiwa na jamii zote zinazohitaji ili wagonjwa wenye kifua kikuu wapate dawa na kupona haraka iwezekanavyo.**

UZUSHI

Wagonjwa pekee wa kifua kifuu ndio wanaweza kushiriki katika utafiti wa kipimo cha kitabibu cha kifua kikuu.

UKWELI

Utafiti wa kitabibu wa kipimo cha kifua kikuu unachunguza kama kipimo kipya cha kifua kikuu kinaweza kubaini ugonjwa huu. Kwa hiyo, watu wote wanaoshiriki katika utafiti huu wa kipimo cha kitabibu cha kifua kikuu watakuwa na dalili za ugonjwa wa mapafu unaoweza kusababishwa na kifua kikuu ama la. **Kipimo hiki kipya kitabaini kifua kikuu tu**, na wale tu watakaobainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huu ndio watakaopewa dawa. Watu wasio na kifua kikuu watapewa dawa nyinginezo.